

102/3

KISWAHILI

Karatasi ya 3

FASIHI YA KISWAHILI

Julai

Saa: 2 ½

MTIHANI WA MAKADIRIO
KIDATO CHA NNE 2010

MAAGIZO

- Jibu maswali manne pekee

- Swali la kwanza ni la lazima

- Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne.

Zilizobaki yaani: Tamthilia, Riwaya, Hadithi fupi na Fasihi simulizi.

- Usijibu maswali mawili kutoka katika sehemu moja.

1. FASIHI SIMULIZI

- a) Ni nini maana ya ngomezi? (alama 2)
- b) Fafanua sifa tano za ngomezi? (alama 5)
- c) Eleza hatua zinazofuatwa wakati wa utegaji wa vitendawili? (alama 4)
- d) Onyesha sifa za vitendawili? (alama 6)
- e) Taja vitanzu vitatu katika kipera cha maigizo (alama 3)

TAMTHILIA

KITHAKA WA MBERIA: Kifo Kisimani
Jibu swali la 2 au la 3.

2. Eleza jinsi ambavyo mbinu zifuatazo zimetumika katika kifo kisimani.

- (i) Jazanda (alama 10)
- (ii) Mbinu-rejeshi (alama 10)

3. “Si vyema kuachilia Butangi kuporomoka. Hatuwezi kuendelea kuahirisha kusuluhisha tatizo hili.”

- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Ni mapendekezo gani yaliyotolewa wakati wa usemi huu kuhusiana na kulitatua tatizo hili (alama 6)
- c) Anayeleta tatizo anaotea Butangi mambo mengi. Yataje (alama 7)
- d) Mwenye kusuluhisha tatizo alipewa ahadi. Zitaje. (alama 3)

4. RIWAYA

S.A Mohammed: Utengano.

Dhihirisha uozo wa kijamii kama unavyojitokeza katika riwaya ya utengano. (alama 20)

5. USHAIRI

SHAIRIA A

Umekata mti mtima
Umeangukia nyumba yako
Umeziba mtohasira
Nyumba yako sasa mafurikoni
Na utahama
Watoto kuwakimbia

Mbuzi kumkaribia chui
Alijigeuza panya
Akalia kuliwa na paka kichwani
Mchawi kuktaka sana kutisha
Alijigeuza simba
Akalia na m'sasi kichwani

Jongoo kutaka sana kukimbia
Aliomba miguu elfu
Akaachwa na nyoka

Hadija wapi sasa utakwenda
Bwanako kumpa sumu?
Hadija umemshika nyoka kwa mkia.
Hadija umepita nyuma ya punda.

SHAIRIA B

Piteni jamani, piteni haraka
Nendeni, nendeni huko mwendako
Mimi haraka. Haraka sina.
Mzigo wangu.mzigo mzito mno
Na chini sitaki kuweka

Vijana kwa nini hampitit?
Kwa nini mwanicheka kisogo?
Mzigo nilioubeba haupo
Lakini umenipinda mgongo na miguu
Na lazima njiegemeze kichwa nchini nendako
Haya piteni piteni haraka!Heei!
Mwafikiri mwaniacha nyuma!
Njia ya maisha ni moja tu
Huko mwendako ndiko nilikotoka
Na nilipopatikikia wengi wenu hawatafika

Kula nimekula sasa mwasema
Niko nyuma ya wakati
Lakini kamamungepita mbele
Na uso wangu kuutama
Ningewambia siri ya miaka mingi

5. a) Haya ni mashairi ya aina gani? (alama 2)
- b) Washairi hawa wawili wanalalamika. Fafanu malalamiko yao. (alama 4)
- c) Onyesha jihni kinaya knavyojitokeza katika tongo hizi mbili (alama 4)
- d) Ni vipi Hadija (alama 4)
- (i) amekata mti mtima
- (ii) amepita nyuma ya punda
- e) Kwa kurejelea shairi 'B' eleza maana ya (alama 4)
- (i) mzigo
- (ii) siri
- (iii) kula nimekula
- (iv) niko nyuma ya wakati

f) Toa mfano mmoja wa uhuru wa ushairi kwa kurejelea mashairi haya. (alama 2)

Hadithi Fupi

K.W Wamitila (Mhariri) Jibu swali la 6 au 7

6. Mti mkuu ukianguka ndege wako mashakani.
Jadili kauli hii ukizingatia hadithi ya mkimbizi (alama 20)

7. a) Eleza matatizo yanayokumba sekta ya elimu ukirejelea hadithi ya Ndimi za Mauti.
(Timothy M. Arege) (alama 10)

b) Eleza sababu zinazothibitisha kuwa hadithi ya Fumbo la Mwana ni fumbo. (alama 10)